


# Jambo la Kufanya ikiwa Mtu Ameonyesha Dalili




Ramani hii ni ya shule za K-12, utunzaji wa mtoto, na shughuli za zaidi ya masomo zilizounganishwa.

## Ikiwa mtu ana mojawapo ya au zaidi ya dalili hizi:

- Homa ( $\geq 38^{\circ}\text{C}$ ) au baridi kali
- Upungufu wa pumzi au matatizo ya kupumua
- Maumivu ya misuli ama mwili
- Hali mpya ya kutohisi ladha ama harufu
- Kikohozi (kipya, kilichobadilika, au kinachozidi)
- Kichefuchefu, kutapika au kuhara
- Uchovu
- Vidonda vya koo
- Kubanika ama mafua\*



## Jitenge nyumbani na upimwe COVID-19



**Watoa huduma ya utunzaji wa mtoto wanafaa kukagua Washington Administrative Code (WAC, Sheria ya Kiutawala ya Washington) yao na mahitaji ya leseni na kufuata hatua zozote za ziada ambazo zinahitajika.**



DOH 820-229 August 4, 2022 Swahili Ili kuomba waraka huu katika muundo mwingine, piga simu 1-800-525-0127. Wateja ambao ni viziwi au wasio na uwezo wa kuzungumza, tafadhali piga simu 711 (Washington Relay) au tuma barua pepe [civil.rights@doh.wa.gov](mailto:civil.rights@doh.wa.gov).

\* Iwapo mtoto yuko chini ya umri wa miaka miwili na amebanwa au ana makasi puani PEKEE bila dalili yoyote nyingine, kipimo na kujitenga hazihitajiki. Dalili za mtoto zikizidi au kuendelea kwa zaidi ya siku tano, fuata ramani ya watoto wa umri wa zaidi ya miaka miwili na inapendekezwa sana uwasiliane na mhudumu wa afya.

\*\* Iwapo huwezi kuvaa barakoa inayokutoshea vizuri: Unafaa kukamilisha kipindi cha siku 10 cha kujitenga nyumbani. Tazama [mwongozo wa utunzaji wa K-12/mtoto](#) ili kupata maelezo zaidi.


# Jambo la kufanya iwapo umepokea taarifa ya mfiduo au ukidhani umekuwa na mfiduo wa COVID-19



Ramani hii ni ya shule za K-12, utunzaji wa mtoto, na shughuli za zaidi ya masomo zilizounganishwa.

## Licha ya hali ya chanjo, tumia miongozo inayofuata:

- Endelea kuhudhuria shuleni, utunzaji wa mtoto, na shughuli.
- Fuatilia dalili kwa siku 10 baada ya mfiduo.
- Unafaa kupimwa haraka iwezekanavyo baada ya mfiduo.
- Unafaa kuvaa barakoa inayokutoshea vizuri kwa siku 10 baada ya mfiduo.



\* Iwapo huwezi kuvaa barakoa inayokutoshea vizuri: Unafaa kukamilisha kipindi cha siku 10 cha kujitenga nyumbani. Tazama [mwongozo wa utunzaji wa K-12/mtoto](#) ili kupata maelezo zaidi.